

# HUDUMA ZA MLIMA WA MOTO NA MIUJIZA

Makao Makuu ya Kimataifa, Lagos, Nigeria.

## KIJIUNGAMANISHA NA TABIBU MKUU

Ufunuo 12:11- \*"Nao wakamshinda kwa damu ya Mwana-Kondoo, na kwa neno la ushuhuda wao; ambao hawakupenda maisha yao hata kufa.

”\*

Katika Jina la Yesu Kristo, mimi ni mtoto mpendwa wa Mungu, Ninaamini Mungu, Ninaamini Yesu Kristo, Ninaamini Mbarikiwa Roho Mtakatifu anayeishi ndani yangu. Naamini katika Nguvu isiyotikisika na ya Milele ya neno la Mungu. Naamini kwamba Mauti na uzima huwa katika ulimi wangu. Ninaamini kuwa ninapofanya ukiri huu katika uzima na uwezo wa ulimi, sawasawa na maneno Bwana ameyatia kinywani mwangu siku ya leo, Nitafanikiwa. Imelandikwa kwamba Yesu alitoa Damu yake kama kinywaji na Mwili wake kama mkate ili yeyote atakayo kunywa na kuumega hatokufa milele. Sasa, Kwa Imani yenye nguvu moyoni mwangu, ninashikilia mkononi mwangu, kikombe chenye Damu ya Mwana Kondoo wa Mungu na ninakunywa, ili niwe na uzima wa milele.

Acha damu itoe ndani yangu, amana zote za uovu wa kurithi na za kujitafutia ndani yangu. Acha isafishe mfumo wa damu yangu. Ninaumega kwa moyo wa Imani, mwili wa Yesu. Kwa kuwa Imelandikwa, mwili wake ni mkate kweli. Naumega sasa ili niumege pamoja naye kwenye Utukufu wake. Ninapokula na kunywa mwili na Damu ya Bwana wangu Yesu Kristo, ninaweka upya agano kati yangu na yeye na kupokea uzima; kwa kuwa Imelandikwa; Uzima upo katika damu. Kwa hiyo, ninapokea uzima na Roho wa Kristo ndani yangu. Amina.

Sifa na Ibada

1. Ahsante Baba kwa faida na msaada wa Damu ya Yesu.
2. Ninatumia damu ya Yesu dhidi ya Magonjwa yote yanayojificha kwenye maisha yangu.

3. Ninanyunyiza damu ya Yesu Kristo kwenye mwili wangu - kutoka utosi wa kichwa changu hadi nyayo za miguu yangu.
4. Ninashika Damu ya Yesu kama ngao dhidi ya kila nguvu ya ugonjwa kwenye maisha yangu,Katika Jina la Yesu.
5. Kupitia Damu ya Yesu,Nimekombolewa kutoka kwa kila ugonjwa.
6. Kupitia Damu ya Yesu,nimeponywa.
7. Kupitia Damu ya Yesu,ninayo uzima wa Mungu ndani yangu.
8. Acha Damu ya Yesu,Isimame kati yangu na kila ugonjwa.
9. Ninalaani kila kazi ya giza kwenye maisha yangu kukauka na mizizi kwa Damu ya Yesu.
10. Ninachora duara wa Damu ya Yesu kunizunguka mimi kinyume cha kila mshale wa udhaifu.
11. Nimeshinda kila udhaifu kwa Damu ya mwana Kondoo.
12. Hakuna roho,mamlaka au falme itakayoweza kuweka ugonjwa wowote juu yangu kwa kuwa nimekombolewa na Damu ya Mwanakondoo.
13. Acha Damu ya Yesu inene uharibifu juu ya kila maendeleo ya uovu kwenye maisha yangu.
14. Acha Damu ya Yesu ,Inene kutoweka juu ya kila udhaifu kwenye Maisha yangu.
15. Acha Damu ya Yesu,inene amani juu ya kila kiungo cha mwili wangu.
16. Acha Damu ya Yesu,inene uponyaji juu ya kila kiungo cha mwili wangu.
17. Ninapooza kila nguvu ya uovu inayopigana na afya yangu.
18. Acha Damu ya Yesu inene kushindwa kwa kila ugonjwa kwenye maisha yangu.
19. Ninafunga nguvu inayokaalisha kila ugonjwa kwa Damu ya Yesu.

20. Ninashika Damu ya Yesu kinyume cha ucheleweshwaji wa kipepo juu ya Uponyaji na Miujiza.

21. Ninashika Damu ya Yesu kinyume cha ukosefu wa afya njema.